Form B7a

RUFIJI BASIN WATER BOARD

# RIPOTI YA KIHAIDROLOJIA
# JARIDA LA MWEZI

## BWAWA LA MTERA

## MEI, 2026

Tarehe ya Utekelezaji: 24 Nov 2025
Toleo, No: 00

# "KILA TONE LINATHAMANI"


**Tarehe ya Utekelezaji: 24 Nov 2025**
**Toleo, No: 00**

# 1 Muhtasari wa Hali ya Maji

Bwawa la Mtera hupokea maji kutoka mito mikuu mitatu: Great Ruaha, Little Ruaha na Kizigo, ambayo ni sehemu ya kidakio cha Great Ruaha. Mito hii ni muhimu kwa uzalishaji wa umeme wa maji, kilimo, matumizi ya majumbani na ikolojia.

Katika mwezi Mei 2026, viwango vya maji vilikuwa juu ya wastani kwa asilimia 143 ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu wa mwezi husika. Hali hii ilisababishwa na wastani wa mvua iliyonyesha katika vidakio pamoja na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji katika kipindi cha Masika (Machi mpaka Mei 2026). Aidha, usawa wa maji katika bwawa la Mtera ulikuwa juu kwa asilimia 100.50 ukilinganisha na wastani wa muda mrefu kwa mwezi Mei.

Upunguzaji wa maji kutoka katika bwawa la Mtera ulianza tarehe 31 Machi 2026 na kuhitimishwa tarehe 14 Mei 2026. Zoezi hilo lilichukua takribani siku 62 na jumla ya mita za ujazo bilioni 1.232 sawa na asilimia 33.30 ya ujazo wote wa bwawa (Billioni 3.7 mita za ujazo) zimepunguzwa katika bwawa.



# Hali ya Hewa

***Hali ya Mvua – Mei 2026:***

Takwimu za mvua zilizorekodiwa na vituo vya hali ya hewa katika maeneo mengi ya Bonde la Rufiji zilikuwa za wastani hadi chini ya wastani, hali hii inachangia kuanza kupungua kwa mtiririko wa maji katika baadhi ya mito hususani ile inayotiririsha maji kwa msimu wa mvua tu.


***Mwelekeo wa Hali ya Hewa – Juni 2026:***

Kwa mujibu wa utabiri wa hali ya hewa uliotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA):


- Unatarajiwa kuwa na vipindi virefu vya ukavu katika maeneo mengi ya Bonde la Rufiji, huku mvua nyepesi zikiendelea kujitokeza mara kwa mara katika maeneo ya Mashariki (Dar es Salaam, Pwani, na sehemu za Morogoro).
- Hali ya joto la wastani hadi baridi kali itaambatana na ukavu katika maeneo ya Kusini na Kati ya bonde.

.


**Utabiri wa Mvua**
**Wiki 01 Juni, 2026**





**Utabiri wa Mvua**
**Wiki 02 Juni, 2026**




**Utabiri wa Mvua**
**Wiki 03 Juni, 2026**




**Utabiri wa Mvua**
**Wiki 04 Juni, 2026**



# Hali ya Mtiririko wa Maji

### Vituo vya Kihaidrolojia


Wingi wa maji mitoni katika kipindi cha mwezi Mei 2026 uliendelea kuwa juu ya wastani wa muda mrefu.Takwimu za vituo vya ufuatiliaji zinaonesha ongezeko la mtiririko ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu (LTA: 2000–2025).

### Matokeo ya Kihidrolojia


Kwa ujumla, mwezi Mei 2026 ulidhihirisha hali nzuri ya rasilimali za maji katika Bonde la Great Ruaha. Mtiririko wa mito ulikuwa juu ya wastani wa muda mrefu, na bwawa la Mtera lilibaki na usawa wa kina cha maji zaidi ya mita 698.70 masl. Hali hiyo imepelekea kuwa na maji cha kutosha kuendeleza shughuli za uzalishaji wa umeme na matumizi mengine ya kijamii na kiuchumi.

**Jedwali 1: Mchanganuo wa Takwimu za Wingi wa Maji**

| Na. | Namba ya Kituo | Mto | Wastani Wingi wa Maji (m3/s) Mei 2026 | Wastani Wingi wa Maji -LTA (Mei) 2000-2025 | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1KA59 | Great Ruaha at Msembe | 79.6 | 51.5 | Juu zaidi ya Wastani |
| 2 | 1KA31 | Little Ruaha at Mawande | 37.2 | 27.1 | Juu ya Wastani |
| 3 | 1KA42A | Kizigo at Chinugulu | 16.7 | 12 | Juu ya Wastani |



# 4 Hali ya Maji Bwawani




**Katika mwezi Mei 2026:**

- Hali ya Usawa na wingi wa maji katika bwawa iliendelea kuwa juu ya uzalishaji umeme (‘Maximum Operational Level)
- Upunguzaji wa maji kutoka katika bwawa la Mtera ulianza tarehe 31 Machi 2026 na kuhitimishwa tarehe 14 Mei 2026. Zoezi hilo lilichukua takribani siku 62 na jumla ya mita za ujazo billioni 1.232 sawa na asilimia 33.30 ya ujazo wote wa bwawa (Billioni 3.7 mita za ujazo) zimepunguzwa katika bwawa.

**Uchambuzi wa Kihaidrologia**

- Kwa ujumla, mwezi Mei 2026 ulidhihirisha hali thabiti ya usimamizi wa Miundombinu ya bwawa na rasilimali za maji.
- Licha ya kupungua kwa wingi wa maji yanayoingia katika Bwawa, kiwango cha maji kilibaki juu ya Maximum Operational Level, na upunguzaji wa maji ulifanyika kwa mafanikio ili kulinda usalama wa bwawa na kuendeleza uzalishaji wa umeme.
- Licha ya kuongezeka kwa mtiririko wa maji katika ukanda wa chini wa bwawa, hakukuwa na taarifa za maafa kwa wananchi wala mifugo yao.
- Hali ya mito ilibaki thabiti na yenye maji ya kutosha kwa matumizi ya kijamii na kiuchumi.

# Mapendekezo







- Kuendelea na Usimamizi shirikishi wa Rasilimali za Maji kuelekea kipindi cha Kipupwe hii itasaidia katika usimamizi thabiti na endelevu wa Bwawa la Mtera pamoja na shughuli za kijamii.
- Kuhakikisha kiwango cha maji kinabaki ndani ya viwango vya juu vya uzalishaji umeme ili kuendeleza uzalishaji wa umeme wa maji kwa ufanisi na matumizi mengine ya maji.

.